# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA KAMATI YA MIFUGO, UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2015l2016.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kwanza kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka huu wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa spika,**

Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kumalizika kwa kazi hii ya Kamati.

**Mheshimwa Spika,**

Kwa upekee kabisa napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa busara na hekima zake kwa mashirikiano na ushauri anaoupata kutoka kwa wasaidizi wake Mhe. Makamu wa

Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kuifikisha nchi yetu mpaka hapa tulipo tukiwa katika hali ya amani na mshikamano jambo ambalo tunajivunia. Lakini pia niungane na wenzangu waliotangulia kumpa pole Rais wa Zanzibar na wafiwa wote kwa msiba uliotokea na Mwenyezi Mungu atawapa subra katika kipindi hiki na tunamuombea marehemu Mungu amlaze mahala pema Peponi. Amiin.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mashirikiano waliyonipa kipindi chote cha kazi za Kamati na hatimaye kufanikisha kazi zetu kwa lengo kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba niwatambue wajumbe wa Kamati hii amabao ni:

1. Mhe.Mlinde Mabrouk Juma - Mwenyekiti
2. Mhe.Abdalla Mohammed Ali - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Asha Bakari Makame - Mjumbe
4. Mhe.Assa Othman Hamad - Mjumbe
5. Mhe.Kazija Khamis Kona - Mjumbe
6. Mhe.Amina iddi Mabrouk - Mjumbe
7. Mhe.Mohammedraza Hassanali- Mjumbe
8. Mhe.Mussa Ali Hassan - Mjumbe
9. Ndg.Himid Haji Choko - Katibu
10. Ndg.Salum Khamis Rashid - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara moja muhimu sana katika nchi yetu ambayo inaratibu na kusimamia sekta mbili kuu ambazo ni sekta ya Uvuvi na sekta ya Mifugo. Sekta hizi licha ya kuwa zinasimamiwa na Wizara hii lakini walengwa na wanaojihusisha na shughuli hizi ni mwananchi wa kawaida ambaye hutegemea shughuli hizi kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,**

Bado ipo haja kubwa kwa Serikali kupitia bajeti yake kuziimarisha sana sekta hizi za Uvuvi na Mifugo kwa kuangalia njia bora na za kisasa ili kuongeza kipato cha

mwananchi wa kawaida na pia kuongeza pato la nchi. Kwani ipo mifano ya nchi nyingi ambazo zimeendelea kwa kutegemea sekta hizo.

**Mheshimwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo naomba niungane na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mafanikio yaliyopatikana katika Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na mafanikio hayo naomba kwa niaba ya Kamati kueleza baadhi ya changamoto ambazo Kamati wamezebaini na kuitaka Wizara izitafutie ufumbuzi kwa ajili ya kuboresha sekta zake na kuongeza la nchi.

**Sekta ya Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,**

Niungane na Waziri kuwa katika kipindi cha mwaka 2014/2015 yapo mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii, lakini bado ipo haja kubwa kwa Wizara hii kuimarisha sekta hii kwani bado suala la ufugaji nchini halijaimarika. Hii ni kwasababu licha ya kuwa uzalishaji wa maziwa umeongozeka kwa asilimia nane 8% uzalishaji wa nyama ya ng’ombe umeongezeka kwa asilimia 3.5% na uzalishaji wa nyama ya mbuzi umeongozeka kwa asilimia 40.9% kutoka mwaka 2013 hadi 2014 lakini bado mahitaji ya maziwa, nyama ya ng’ombe na nyama ya mbuzi ni makubwa ukulinganisha na matumizi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanya takwimu hizo za uzalishaji lakini bado Kamati inamashaka na upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji wa maziwa, nyama ya ng’ombe na nyama ya mbuzi kwasababu Kamati inaamini kuwa yapo maeneo mengi sana hapa Zanzibar ambayo yanafanya shughuli hizo na taasisi hii haipati takwimu zake. Kwahiyo Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuandaa utaratibu mzuri ambao utasaidia kupatikana kwa takwimu sahihi ambazo zitasaidia katika uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara inayo eneo kubwa sana Pangeni ambalo lipo kwa ajili ya shughuli za Ufugaji, lakini bado kamati inasikitishwa sana kwa kutokutumiwa eneo hilo ipasavyo ili kukuza sekta hii ya Mifugo nchini, Kamati inaendelea kuitaka Serikali

kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuangalia namna ya kulitumia eneo hilo kwa ajili ya shughuli za Ufugaji ili kuimarisha sekta hii nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inaendelea kumpongeza mwekezaji mzalendo ndugu Said Salum Bakhresa kwa kuanzisha kiwanda cha kuzalisha maziwa, Kamati yetu inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kufanya mazungumzo na mwekezaji huyu ili kuekeza katika ufugaji wa ng'ombe na tuweze kuzalisha maziwa hapa hapa badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi. Kufanya hivyo ni kuimarisha ufugaji, kuinua kipato cha mfugaji lakini pia ni kuinua uchumi wa nchi kwasababu bidhaa tutakuwa tunazalisha wenyewe ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha kituo cha ukusanyaji maziwa ambapo kiasi cha Shilingi Milioni Arubaini na Mbili (42,000,000/=) zimetengwa kwa ajili ya ya kuanzisha kituo hicho. Kuanzishwa kwa kituo hiki kutazidi kuimarisha ongezeko la uzalishaji wa maziwa yaliyobora hapa nchini. Licha ya kuanzishwa kwa kituo hiki kamati yangu inataka kujuwa jee kituo hiki kitakuwa kazi yake ni kukusanya maziwa tu kutoka kwa wafugaji na kuyauza au kutakuwa na vifaa vya kupimia ubora wa maziwa yanayoletwa kabla ya kuyakusanya? Lakini pia Kamati inashauri Serikali itoe vipaombele katika kutafuta njia za kusarifu bidhaa ya maziwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Taaluma kwa wafugaji ni jambo la msingi sana ili kuzalisha maziwa yenye viwango na yaliyobora na yatakayoweza kuingia katika soko. Ipo haja kwa Wizara hii kuendelea kutoa elemu kwa wafugaji kwani bado inaonekana taaluma ya wafugaji haijaenea kwa wafugaji jambo ambalo husababisha kutokuimarika kwa shughuli za ufugaji hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakati Serikali ikijiandaa na kuboresha sekta ya Mifugo nchini ambapo katika bajeti ya mwaka huu jumla ya Shilingi Bilioni moja, milioni mitatu kumi na sita laki tatu na elfu Ishirini na Tisa (1,316,329,000/-) zimetengwa kama ni Progaramu

Kuu kwa ajili ya Maendeleo ya Mifugo. Hata hivyo Kamati yangu inaendelea kuishauri sana Wizara wakati ikijiandaa kuboresha sekta ya Mifugo kwa kuongeza idadi ya mifugo pia iangalie sana suala la kuimarisha upatikanaji wa chakula na lishe bora kwa mifugo ambapo shughuli hii ya Kuimarisha upatikanaji wa chakula na ulishaji bora imewekewa kiasi cha Shilingi Milioni tano laki tisa na elfu kumi na mbili (5,912,000/-) katika bajeti ya mwaka huu. Kamati yangu inaishauri Serikali kuliangalia vizuri sana eneo hili ili liende sambamba na ongezeko la mifugo, isiwe tunaboresha kuongeza mifugo lakini chakula cha mifugo hiyo hakipatikani hapo itakuwa hatujaboresha sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Bajeti ya Mwaka huu Wizara imetenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kuboresha utafiti wa maradhi ya wanyama pamoja na matibabu, lakini suala la matibabu ya wanyama nalo pia ni la msingi sana kwani na linahitaji kuangaliwa kitaalamu zaidi ili kunusuru sekta hii ya mifugo, kwani maradhi kwa wanyama yanaweza kuleta athari kubwa sana kwa wafugaji na kurudisha nyuma sekta ya mifugo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kupitia sekta hii ya Mifugo juhudi za kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za Ufugaji lakini bado ipo haja kwa Serikali kutokuridhika na mapato hayo yanayokusanywa na badala yake Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya fedha iangalie namna ya kuongeza vianzio vya kukusanya mapato ambapo Kamati yangu inaamini vianzio hivo vitapatikana baada ya kuiboresha sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Bajeti ya mwaka huu Wizara imetenga kiasi cha Shilingi Milioni Mia Moja na Arubaini na saba, Laki Mbili na Themanini na nne elfu (147,284,000/=) kwa ajili ya Mradi wa kudhibiti kichaa cha mbwa. Kamati inakubaliana na Mradi huu ambao kila mwaka unaombewa fedha, lakini bado tunasikitishwa sana na matokeo yanayoendelea kuripotiwa kila siku ya watu kutafunwa na mbwa na uzururaji ovyo wa mbwa. Kamati inaitaka Serikali kuchukuwa hatua ili kukabiliana na tatizo hili

la uzururaji ovyo wa mbwa ambalo hupelekea watu kutafunwa na mbwa mara kwa mara.

**Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,**

Zanzibar ni visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari, kwahivyo ni wazi kuwa sekta ya Uvuvi ni moja ya Sekta muhimu sana katika kuinua uchumi wa Zanzibar kwasababu rasilimali ya nchi yoyote ya visiwa ni bahari. Zipo nchi kadhaa ambazo zimeendelea kwa kutegemea bahari kupitia sekta ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inashuhudia jitihada nyingi zinazofanywa na Serikali ili kuinua sekta ya Uvuvi nchini lakini bado inaendelea kusikitishwa sana kwa kuchelewa kuimarishwa kwa sekta hii kwani kuchelewa kuimarishwa kwa sekta hii ni kuikosesha nchi mapato mengi ambayo yangeliweza kupatikana na yangelisaidia sana kuinua uchumi wa nchi yetu. Kuchelewa kuimarisha sekta ya Uvuvi ni kutoithamini na kuipoteza rasilimali yetu ya bahari ambayo kama itatumiwa ipasavyo ingelisaidia sana kuongeza mapato ya nchi na ajira kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaeleza kuwa uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 30,712 zenye thamani ya Shilingi Bilioni mia moja na kumi na moja, mia nane sabiini na mbili milioni laki tisa na thelathini na tisa elfu mia saba na arobaini (111,872,939,740/=) kwa mwaka 2013 hadi kufikia tani 32,973 kwa mwaka 2014 zenye thamani ya Shilingi Bilioni mia moja na ishirini na sita,mia tisa ishirini na tatu milioni, laki moja elfu sabiini na mbili na hamsini na tau (126,923,172,053/=). Pamoja na takwimu hizi zilizotolewa na Wizara bado Kamati yangu inamashaka na usahihi wa takwimu hizi kwani bado yapo maeneo mengi ya Uvuvi ambayo hayafanyiwi takwimu. Aidha kwasababu ya kukosekana kwa vifaa au uhaba wa wafanyakazi. Kwahivyo Kamati inaendelea kuitaka Wizara kuhakikisha inaweka utaratibi mzuri ili kuhakikisha kwamba takwimu za uzalishalishaji wa samaki zinapatikana kila pahala jambo ambalo litasaidia sana kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuweza kujitathmini vizuri katika suala la Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,**

Jambo jengine ambalo Kamati ingelipenda kulizungumzia na pia kuitaka Serikali ifanye kila jitihada ihakikishe kuwa inalifanikisha ni kuzuiya Uvuvi haramu kama ilivyofanikiwa kuzuiya magendo ya karafuu. Serikali haitakiwi kulifumbia macho suala hili kwani athari zake ni kubwa sana katika uchumi wa nchi kwasababu huharaibu mazingira ya bahari na mazilio ya samaki lakini pia tunapoteza mapato ya nchi. Katika bajeti ya mwaka huu wa fedha katika Programu ya Maendeleo ya uvuvi na Uhifadhi moja ya shughuli zake ni ***Kuimarisha doria shirikishi katika maeneo ya hifadhi za bahari*** ambapo kiasi cha Shilingi Milioni Ishirini na Nane na Laki Nane (28,800,000/=) zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hiyo. Kamati inaiomba sana Serikali kuna haja ya kuimarishwa zaidi eneo hili ili kukomesha suala hili la Uvuvi haramu.

**Mheshimiwa Spika,**

Itakumbukwa kuwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walizungumzia sana kuhusu suala la kuanzishwa kwa Uvuvi wa Bahari Kuu, katika bajeti ya mwaka huu Serikali imeomba kuidhinishiwa fedha kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu ambao utagharimu jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nne na Tisini na Tatu, Laki Tisa na Elfu Kumi na Saba (11,493,917,000/=) ambapo katika Mradi huu kutakuwa na shughuli zifuatazo:

- Kujenga soko la samaki pamoja na diko la Uvuvi
- Kusomesha wavuvi masuala ya uvuvi wa bahari kuu
- Mradi wa kuendeleza uvuvi kwa ukanda wa Kusini Magharibi
- Ujenzi wa soko la Malindi/Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu, ambapo shughuli hii ya mwisho imetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni Nane (8,000,000,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu katika Mradi huu itamuomba Mheshimiwa Waziri baadae kutoa ufafanuzi au mchanganuo kwenye fedha zilizotengwa katika shughuli ya mwisho ambayo ni Ujenzi wa soko la Malindi/Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu, ambapo shughuli hii imetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni Nane (8,000,000,000/=). Kwasababu shughuli hii imebeba shughuli mbili kubwa na zote zimewekewa fedha

kwa pamoja kwahivyo tunamomba Waziri atoe ufafanuzi ni shilingi ngapi zitatumika kwa ajili ya Ujenzi wa soko la Malindi na shilingi ngapi zitatumika kwa ajili ya Uimarishaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu. Lakini pia Kamati itamuomba Waziri kutueleza jee katika kuimarisha suala hili Wizara imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya ununuiz wa vifaa zikiwemo meli kwa ajili ya Uvuvi wa bahari kuu.

**Mheshimiwa Spika,**

Uwekezaji katika Uvuvi wa Bahari Kuu ni suala ambalo limekuwa likumzungumzwa sana, kuna nchi ambazo zimekuwa zikizungumzwa kuwa zinayo nia ya kutaka kuekeza katika Uvuvi wa Bahari Kuu hapa Zanzibar kwa mfano Misri, Madacsca na nchi nyengine, Kamati yangu pia itamuomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kuhusu suala hili la uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu jee limefikiwa hatua gani mpaka sasa hivi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kutaka kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu, Kamati inaiomba sana Serikali ifanye jitihada za kuharakisha kuanzishwa kwa suala hili kwani limekuwa likizungumzwa kwa mda mrefu sana katika Baraza hili. Ni wazi kuwa hali ya uchumi itabidilika na pato la nchi litaongezeka pale Serikali itakapoanzisha na kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu. Kamati yangu inaiomba sana Serikali katika mwaka huu wa fedha shughuli hii ianze ili tuweze kutumia rasilimali zetu kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kueleza baadhi ya mafaniko katika utekelezaji na changamoto zilizomo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati yangu ilipitia na kuijadili Bajeti ya Wizara hii ambayo imekuja katika mfumo mpya wa PBB ambapo kwa kiasi kikubwa tulipata changamoto ya kuijadili bajeti hii kutokana na upya wa mfumo huu lakini hata hivyo hatimae kamati iliichambua ilitoa maoni yake na kuipitisha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Mapato, katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 Wizara ya Mifugo na Uvuvu inakadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa na

Hamsini na Sita, Laki Tatu na Sitini na Mbili Elfu (956,362,000/=). Kamati yangu inaipongeza sana Wizara kwa kufikia makadiro hayo ukilinganisha na Makadirio ya Mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo fedha zilizokadiriwa kukusanywa mwaka huo ni jumla ya Shilingi Mia Sita na kumi na Tatu Milioni (613,000,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaendelea kuikumbusha Serikali kuboresha sekta zinazosimamiwa na Wizara hii ili kuongeza mapato yatokanayo na sekta hizo, Kamati inaamini kuwa kuboresha sekta hizo ***sio kupoteza bali ni kuekeza*** na mafanikio yake yataonekana katika kipindi kifupi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kuwa kwa upande wa Matumizi Wizara ya Mifugo na Uvuvi fungu MO1 itakuwa na Programu Kuu tatu na Programu Ndogo saba, ambazo ni hizi zifuatazo:

Progaramu ya Kwanza ni **Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo** ambayo jumla ya Programu hii ni Shilingi Bilioni Moja, Mia Tatu Kumi na Sita Milioni, Laki Tatu na Elfu Ishirini na Tisa (1,316,329,000/=). Katika Programu hii zipo Programu Ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo ambapo jumla yake ni Shilingi Mia Sita Milioni, Laki Mbili na Hamsini na Tisa Elfu (600,259,000/=) na Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ambapo jumla yake ni Shilingi Mia Saba Kumi Sita Milioni na Sabiini Elfu (716,070,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuwa wakati Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakapo muidhinishia fedha kwa ajili ya Programu Kuu hii akumbuke shughuli zifuatazo ambazo ameziombea fedha hizo ahakikishe kuwa zimetekelezwa kama Wizara ilivyojipangia venginevyo aandae majibu mazuri ya kuwaambia Wajumbe wa Baraza lako tukufu, naomba nizitaje shughuli zenyewe ni: Kuimarisha tafiti shirikishi kwa wafugaji, Kuimarisha upatikanaji wa chakula na ulishaji bora, Kuimarisha huduma za ugani na ubora wa maziwa, Kuimarisha huduma ya ugani kwa jamii, Kudhibiti maradhi yanayoenezwa na kupe, Kudhibiti

magonjwa ya kuku na jamii ya ndege, Kudhibiti maradhi ya minyoo na koksidia na Kuimarisha huduma za uchunguzi wa maradhi.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya Pili ni **Programu Kuu ya Maendeleo na Uvuvi** ambapo jumla ya Programu hii ni Shilingi Mia Sita Arubaini na Tatu Milioni, Laki Tano na Thelathini na Mbili Elfu (643,532,000/=). Katika Programu hii zipo Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini ambayo jumla yake ni Shilingi Mia Mbili na tatu Milioni, Laki Nane na Kumi na Moja Elfu (203,811,000/=) na Programu ndogo ya Pili ni Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi ambapo jumla yake ni Shilingi Mia Nne na Thelathini Tisa Milioni, Laki saba na Ishirini na Moja Elfu (439,721,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Ili Programu hii iweze kutekelezeka Mheshimiwa Waziri ameomba kuidhinishiwa fedha hizo katika shughuli zifuatazo: Kuimarisha huduma za ugani kwa jamii, Kuimarisha upatikanaji wa vifaranga vya samaki, Kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini, kuimarisha kilimo cha shughuli za mwani Zanzibar, Kuimarisha doria shirikishi katika maeneo ya hifadhi za bahari na Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira. Kamati yangu inaamini kuwa shughuli hizo zilizomo ndani ya program hii ni za msingi sana na Wizara itazitekeleza ipasavyo baada ya kuidhinisiwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya tatu ni **Programu Kuu ya Utawala wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi** ambayo imetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni Mbili, Mia themanini na saba Milioni, Laki tano thelathini na tisa Elfu (2,187,539,000/=). Program hii inazo Programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo ya Utawala na Mafunzo ambayo ni jumla yake ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni Kumi, Laki Tatu na Sabiini na saba Elfu (1,010,377,000/=), Programu ndogo ya pili ni Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ambayo jumla yake ni Shilingi Mia mbili na Sita Milioni, Laki Tisa na Elfu Sitini na moja (206,961,000/=) na Programu ndogo ya tatu ni Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba jumla yake ni Shilingi Mia Tisa Sabiini Milioni, Laki mbili na Elfu moja (970,201,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa shughuli hii Mheshimiwa Waziri ameomba kuidhinishiwa fedha hizo katika shughuli zifuatazo: Kutoa huduma za kiutumishi za Wizara, Kuwajengea uwezo wa Kitaaluma kwa wafanyakazi, Kuandaa na Kuratibu mipango ya Wizara, Kuratibu shughuli za utafiti za Mifugo na Uvuvi, Kutoa huduma za utumishi za Wizara – Pemba, Kuwajengea uwezo wa Kitaaluma kwa wafanyakazi – Pemba na Kuratibu shughuli za mipango ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Pemba. Kamati yangu inakubalina na shughuli hizi za kiutawala ambazo zikitekelezwa ipasavyo basi zitasaidia sana kuimarisha sekta za Mifugo na Uvuvi zillizopo chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kumalizia hotuba yangu nawaomba sana Wajumbe wenzangu wa Baraza hili, kwa kuwa sasa hivi tupo katika mfumo mpya wa Bajeti unaotumia Programme Based Budget (PBB) tuangalie kwa umakini sana katika Shughuli ambazo zipo katika kila Programu kwasababu mwisho wa siku kupitia hizo shughuli ndipo Baraza hili litakuja kusema kuwa Programu tuliyoiidhinishia fedha imetekelezeka au haikutekelezeka na vile vile katika hizi shughuli ndipo ambapo tutapata nafasi ya kumuhoji Waziri utekelezaji wa Programu iliyopo chini ya shughuli hizo. Na ndio maana katika hotuba yangu hii nimeona niziorodheshe shughuli hizi kwa kila Programu Kuu ili Wajumbe wa Baraza hili wapate nafasi ya kuchangia, kutoa maoni yao na pia kumuhoji Waziri juu ya Programu hizi anazoziombea fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba yangu kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii kwani imebeba sekta muhimu sana za nchi yetu ambazo ndio mategemeo makubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kuwasilisha.

…………………

**ABDALAA MOHAMMED ALI,**
**MAKAMU MWENYEKITI,**
**KAMATI YA MIFUGO, UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI,**
**BARAZA LA WAWAKILISHI.**
**ZANZIBAR.**